

## **TAWA YAFANYA WARSHA YA SIKU MOJA KWA KAMPUNI ZA UWINDAJI WA KITALIII KUHUSU UTARATIBU WA KUGAWA VITALU VYA UWINDAJI WA KITALII KWA NJIA YA MNADA WA KIELEKTRONIKI**

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii ilifanya warsha ya siku moja tarehe 22 Februari 2019 Jijini Arusha. Bw. Imani R. Nkuwi, Naibu Kamishna, Utalii na Huduma za Biashara kutoka TAWA alifungua warsha hiyo iliyohusisha kampuni za uwindaji kitalii nchini. Lengo la warsha ilikuwa ni kuwasilisha mwongozo wa kugawa vitalu kwa njia ya mnada wa kielektroniki *Guidelines for the allocation of hunting blocks through auctioning* pamoja na kuzifundisha kampuni za uwindaji wa kitalii namna ya kutumia mfumo wa kielektroniki (**MNRT Portal**) wa kugawa vitalu kwa njia ya mnada.

Jumla ya washiriki **56** kutoka kampuni **30** za uwindaji wa kitalii walishiriki. Warsha ilifanyika kwa ufanishi mkubwa na washiriki walionesha kuridhishwa na hatua iliyofikiwa na serikali katika maandalizi ya ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa njia ya mnada. Kampuni zilizoshiriki zimeomba serikali kuhakikisha kuwa mnada wa vitalu unafanyika mapema iwezekanavyo ili kampuni zitakazoshinda ziweze kuuza safari katika masoko (hunting conventions) ya Ulaya na Falme za Kiarabu.

Washiriki wamepongeza juhudi za serikali katika kuandaa utaratibu wa kugawa vitalu kwa njia ya kielektroniki na wanaamini kuwa utaratibu huo utatoa fursa sawa kwa kampuni zote wakati wa kugawa vitalu.

Aidha, Mamlaka imepanga kugawa vitalu vilivyo wazi kwa njia ya mnada wa kielektroniki baada ya taratibu zote za kisheria kukamilika.

